



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI



*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb.Na. HW/S.1/VOL/III/29**

02 Septemba, 2021

## **TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni anawatangazia nafasi ya kazi na anakaribisha maombi kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya kazi ya Mtendaji wa Kijiji kama ifuatavyo:

### **1. Nafasi ya kazi: MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI MOJA (1)**

#### **SIFA ZA MWOMBAJI**

Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo;- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### **KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III**

- i. Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika Kijiji.
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha Wataalam waliopo katika Kijiji.
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- xi. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji.

#### **MSHAHARA**

Kwa kuzingatia Waraka wa mishahara wa Serikali ngazi ya TGS B1




## MASHARTI YA KAZI/WAOMBAJI KWA UJUMLA

- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45.
- Waombaji ambao ni Watumishi wa Umma na wana sifa za kuingilia wapitisho barua zao za maombi kwa Waajiri wao.
- Nafasi inayoombwa iandikwe katika kichwa cha habari cha barua.
- Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Adetailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
- Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma na mafunzo kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali:
  - Cheti cha kuhitimu Kidato cha IV au VI.
  - Cheti cha mafunzo ujuzi NTA -5.
  - Cheti cha kuzaliwa.
  - Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni na iandikwe jina nyuma.
- "Testimonials", "Provisional results", "Statement of results", Hati za matokeo ya kidato cha IV na VI (form IV and form VI results slips) **HAVITAKUBALIWA**
- Waombaji waambatishe na nakala ya kitambulisha cha Taifa au Namba ya kitambulisho cha NIDA kwa wasio kuwa na kitambulisho.
- Waombaji waliosoma nje ya nchi waatishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA na TCU).
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi zitapelekea wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.
- Waombaji watakaokidhi sifa ndio watakao itwa kwenye usahili.
- Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe kwa njia ya posta au kuwasilishwa moja kwa moja katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni sehemu ya Masijala ya Wazi kwa anuani ifuatayo:

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S.L.P 60,  
MANYONI.**

- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **16/09/2021** Saa **9:30** alasiri. Tangazo pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri: **[www.manyonidc.go.tz](http://www.manyonidc.go.tz)**, **mbao za matangazo** na tovuti ya Sekretarieti ya Ajira: **[www.ajira.go.tz](http://www.ajira.go.tz)**

Tangazo hili limetolewa na;



Kennan Jey Kidanka

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI**